



# Nitakuwa na furaha kama... nitapenda haki!

"Heri wenye njaa na kiu ya haki maana hao watahibishwa" (Mt 5,6)



## Lengo

Kutambua hali za kila siku ambazo kwazo tunaweza kung'amua na kuhakikisha haki na kuwa na ufahamu wa jukumu letu.



## Mambo yaliendaje?

Mwanzoni kuna sehemu ya makaribisho, ambapo inabidi kuacha nafasi ya mazungumzo na mawasilisho ya kile ambacho kila mtu ameishi, mang'amuzi na magumu pia. Kukaribisha maana yake ni kumfanya kila mtu ajisikie nyumbani: ubunifu utatusaidia kupata mbinu zinazofaa. Pia tunaweza kujikumbusha malengo tuliyojiwekea kwenye mkutano wa mwisho: "ulikuwaje?"



## Shughuli ya utambulisho

« UPANDE WA HAKI »

**MUDA:** kama dakika 45

**VIFAA:** post-it, karatasi kubwa, kalamu, picha zilizopigwa awali, na kundi la hali za dhuluma katika mji wenu.

**UENDESHAJI:** Mapema kabla ya mkutano (wiki au siku chache) waombe watoto wapige picha ya hali ya kudhulumu waliyoiona katika mji wao. Hapa ni baadhi ya hali ziwezekanazo: Watoto ambao hawana haki ya elimu, wakimbizi wanaotoroka vita, wakosa makazi, uonevu, rundo la takataka, kununua bidhaa za bei nafuu ambazo wazalishaji hawalipwi kwa haki, kunakili kutoka kwenye kitabu wakati wa mtihani darasani, nk .... tuanze mkutano kwa kushirikisha ambapo kila mtu anawasilisha tukio lake na hatimaye kusema jinsi alivyohusika alipokutana nalo (alipata hisia gani, mawazo gani, alitamani kuwe na mabadiliko?). Inawezekana kumalizia kwa kuchora picha kubwa: "kipimajoto cha haki katika mji wetu". inawezekana kuleta maneno ya msingi yaliyotokana na baadhi ya maswali: "Ni nini wananchi wanaweza kufanya ili kusaidia kuhakikisha haki?" - "Ni nini taasisi zinaweza kufanya?" - "Mimi ninaweza kufanya nini?"

**HITIMISHO:** Katika awamu ya mwisho ya majadiliano, wakaribishe wavulana au wasichana kwenye mazungumzo na tafakari juu ya maisha yao ya kila siku na tabia ambayo inaweza kurekebishwa au kuongezewa bidii, ili kujichukua kama wananchi watendaji walio katika "upande wa haki." Kila mmoja anaweza kuchukua jukumu la kutekeleza shuleni, kwenye jamii, katika familia....



Tuishi hivi



Nitakuwa na furaha kama...  
nitapenda haki!

**S**huleni, mwalimu haku-  
gundua kosa nililolifanya  
kwenye kazi niliyoifanya da-  
rasani. Niliona afadhali ku-  
mwambia kwa sababu nilio-  
na si haki kupata maksi zaidi  
ya nilizostahili.

Rafiki zangu walinishauri  
nisimwambie, lakini mimi  
nilifikiri kuwa hii pia ni nafasi  
ya kushuhudia Injili. Mwalimu  
alinishukuru kwa uaminifu  
wangu na kwa mshangao  
mkubwa, aliniongezea maksi  
kama zawadi kwa sababu  
ya tabia yangu. Imani yangu  
ilinipa furaha kubwa na pia  
kwa rafiki zangu.

*(M. – Costa Rica)*




Kwa undani

### «HAKI YA KWELI»



*Chiara Lubich, Kongamano la gen 3,  
heri, 20 Juni 1975*

**L**eo haki inazungumziwa sana, la-  
kini tuwe makini kwa sababu haki  
ya kweli ni kumpenda Mungu na kumpenda Ji-  
rani: kwa sababu Mungu alitupatia kila kitu na  
sisi pia tunapaswa kumpatia kila kitu, moyo,  
akili, nguvu; wanadamu kwa sababu ni ndugu  
zetu. Wale walio na njaa na kiu ya haki ni wale  
wasiojipa amani mpaka kutakapokuwa na haki  
ya kweli duniani, yaani mpaka Mungu atakapo-  
pendwa kuliko vitu vyote na mpaka wanadamu  
watakapopendana kati yao. Halafu gen, tuta-  
shibishwa kwa sababu Mungu atatupatia mara  
mia, nyumba, ndugu, mali, kama ilivyotokea  
kwa watakatifu ambao zaidi walivyotoa kila kitu  
kwa Mungu na kugawanya mali zao na ndugu  
zao na masikini, ndivyo walivyopata riziki zaidi  
na kando kando yao kila mtu alikuwa na mkate  
wa kula na furaha ya Mungu. 

**Nota:**

Kwenye tovuti <http://assistentigen3.focolare.org>  
video pia inapatikana



Kwa ajili ya mlezi



## Tathmini baada ya mkutano

- Shughuli zilizopendekezwa zilikuza mvuto wa vijana kwa hii heri?
- Kuna eneo la pekee lililojitokeza ambalo gen 3 wanaona kuwa ni vigumu kutekeleza haki?
- Walichukua dhamira gani ili kuiishi? Lengo liwe kuwaongoza na kuwasaidia katika pendekezo lao hadi mkutano ujao.
- Nafikiri kuwa mada imekamilika au nadhani kuwa kuna kitu kinachokosekana cha kukijadili katika mkutano ujao?
- Kuna magumu yaliyojitokeza? Nini ni muhimu kukumbuka ili kuboresha wakati ujao?